2. Kusudi lao na ofisi katika uumbaji lilikuwa lipi? Zaburi 34: 7; Waebrania 1:13, 14.
3. Je, Muumba analo fikira kuwa mwanadamu ni wa familia moja kama malaika? Waefeso 3:14, 15; Ufunuo22:8, 9.
4. Je, familia hii ina jina sawa na ni jina gani? 1 Wakorintho 15:9; 1 Wathesalonike 2:14.
5. Ni nini imesemwa kuhusu malaika wa Mbinguni kuhusu amri? Zaburi 103: 20.
6. Ni kwa njia gani wajumbe hawa wa Mbinguni huitwa kwa msaada wetu? Mathayo 26:53.
7. Wakati Petro alikuwa amefungwa kwa minyororo miwili gerezani, jinsi gani alifanywa kuwa huru? Matendo ya Mitume 12:7-10.
8. Ni kupitia kwa maombi ya nani yeye alipata kusaidiwa?. Mstari wa 5.
9. Jinsi gani inawezekana kwa haraka kwake Mwenyezi Elohim kusikia maombi yetu, na kuyajibu? Danieli 9:21.

**Maelezo:** Malaika huitwa kwa msaada wetu wakati tunapoomba. Maombi ni kiungo kinachotuunganisha ambacho kinatupea nguvu takatifu za uweza ambazo ni lazima tuwe nazo ili tuishi maisha ya ushindi.

10. Ni uhusiano gani muhimu upo kati ya mtu na malaika, unaohusu uelewaji wa maandiko? Danieli 9:22.
11. Katika maumivu makuu ya Gethsemane, jinsi gani Baba wa Mbinguni alipeana msaada wa wake katika saa hii ya shida? Luka 22:43.
12. Jinsi gani tutapata msaada wa kiroho? Mathayo 7:7, 8.
13. Malaika wa Mbinguni wana nia katika masuala ya binadamu? Luka 15:10.



3. Kwa nini Paulo alisema alikuwa na wivu juu ya wafuasi wake? 2 Wakorintho 11:1-3.
4. Ni nini kilichosababisha Anania kutenda dhambi? Matendo ya Mitume 5:3.
5. Tunafaa kuwa na uhusiano wa karibu na waovu? Mithali 23:6, 7.
6. Kwa nini tunahitaji msaada wa Elohim katika vita vyetu dhidi ya dhambi? 2 Wakorintho 10:4, 5.
7. Je, tunahitaji msaada kwa ajili ya sababu nyingine? Waefeso 6:12.
8. Ni kwa nani injili inaweza kuwa imesitirika? 2 Wakorintho 4:3, 4.
9. Ni nani ambao ni mbegu zilizotupwa njiani? Mathayo 13:19.
10. Ni nini lazima waumini wote wapitie? Waefeso 2:2, 3.
11. Ni kwa nini tuna uwezo wa kushinda mkuu wa ulimwengu huu? 1 Yohana 4:4.
12. Kwa nini tunaambiwa tuthibitishe upendo wetu kwa Mwokozi? 2 Wakorintho 2:8-11.
13. Ni nini lazima muumini anafaa kuangalia kwa nyakati zote? Zaburi 19:13, 14.
14. Ni nini lazima tufanye ili Mwokozi aje kwetu? Ufunuo 3:20.
15. Je, ni hatua ipi nyingine tutachukua? Yakobo 4:6-8.
16. Ni ujumbe upi ulikuwa wa kwanza Mwokozi alihubiri ? Mathayo 4:17; Mathayo 10:32.
17. Ni nani hawezi kuwa mwanafunzi wa Yahshua? Luka 14:26, 27, 33.

*******************************





***"Utakieni Yerusalemu amani; Na wafanikiwe wakupendao." Zaburi 122:6***



# Masomo ya Bibilia

***kwa ajili ya***

**KANISA LA ELOHIM (COG)**
**Siku Ya Saba (7th Day)**

Robo Ya Tatu
2017

KWA AJILI YA
Julai, Agosti, Septemba.

Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache ....

**Tuma maombi yote kwa S.L.P 568, Jerusalem — Israel**

**Somo La Julai 29, 2017.**

## NI NANI AMBAYE TUTATII

**Somo Kuu: Matendo 5:12-27.**
**Fungu La kukariri: Matendo 5:29.**

1. Ni pendekezo gani iliwekwa kwa Israeli katika mlima wa Sinai? Kutoka 19:3-6.
2. Ni nini ingewafuata wana wa Israeli kama wangetii amri hizi? Kumbukumbu la Torati 11:26, 27.
3. Licha ya ahadi hizi ambazo ni nzuri sana, jinsi gani wana wa Israeli walilifikiria hilo agano? Yeremia 31:31, 32
4. Ni somo gani tunaweza kujifunza kutoka kwa mtazamo wa Shadraka, Meshaki, na Abednego wakati wa jaribio? Danieli 3:8-26.

**Maelezo:** Hebu tuelewe kwamba hakukuwa na uhakika wa kuokolewa, lakini waliridhika kufa katika kumtii Bwana.

5. Ni nini kilichosemwa kuhusu kutii Bwana Yahshua katika Waebrania 5:7-10?
6. Ni nani mwingine tunafaa kutii licha ya Bwana, na ahadi ya Elohim kwa ajili ya utiifu huu ni nini? Mithali 23:22; Waefeso 6:1-3.
7. Nani ambaye tunapaswa kutii katika Kanisa? Waebrania 13:17; 1 Wathesalonike 5:12, 13.
8. Ni heshima kiasi gani wao wanastahili, na tunafaa kuamini mashtaka yote? 1 Timotheo 5:17-19.
9. Nani ambao tunapaswa kutii nje ya Kanisa? Tito 3:1.
10. Mtazamo wetu kwa wanaotawala ni upi? 1 Timotheo 2:1-3;1 Petro 2:12-19.



aliyeziumba mbingu na dunia. Ilikuwa pia saa ya hukumu juu ya taifa la Kiyahudi (Luka 21:24), na juu ya mkuu wa ulimwengu huu.

4. Ni nini imesemwa kuhusu wakati wa hukumu ambayo ilikuwa sehemu ya ujumbe wa kwanza kwa dunia yote? 1 Petro 4:17; Yohana 16:7-11; 12:31.
5. Ni nini asili ya ujumbe wa malaika wa pili? Ufunuo 14: 8.
6. Ni nini asili ya ujumbe wa malaika wa tatu, na ni juu ya nani hasa umeelekezwa moja kwa moja? Ufunuo14:9, 10.
7. Je, ni tukio gani linalofuata ujumbe huu? Kuna ujumbe mwingine bado utapeanwa, au ni wakati wa mfalme kuja na kutawala? Ufunuo 14:14-16.
8. Je, Ufunuo 15:1 pia inatuambia nini kuhusu mapigo haya ya mwisho?

**Maelezo:** Ujumbe wa kumtambua mnyama, na kutoa tahadhari hii, ni "chakula wakati unaofaa". Ni ujumbe huu ambao umefika wakati wake katika ulimwengu kwa wakati huu maalum.

*******************************

**Somo La 9 Septemba, 2017.**

## UUMBAJI WA JUU

**Somo Kuu: Waebrania 1**
**Fungu La Kukariri: Waebrania 1:14.**

1. Ni uumbaji upi wa viumbe ambao ni sawa na mwanadamu, hali yetu ikilinganishwa na wao ni ipi? Zaburi 8:3-5.



**Somo La Julai 1, 2017.**

## WANAWALI KUMI

**Somo Kuu: Mathayo 25: 1-13.**
**Fungu La Kukariri: 1 Wakorintho 16:13.**

1. Mwokozi alifananisha ufalme wa Mbinguni na nini? Mathayo 25: 1.
2. Wanawali kumi walikuwa na tabia zipi ambazo zilikuwa sawa? Mathayo 25: 1 (sehemu ya mwisho).
3. Jinsi gani wale wapumbavu walionyesha upumbavu wao? Mathayo 5:3.
4. Jinsi gani wale wenye busara walionyesha hekima yao? Mathayo 25: 4.

**Maelezo**: Tunaona ya kwamba wote kumi walikuwa wanawali. Hii inaashiria usafi wa tabia. Wanawakilisha Kanisa ambalo lamsubiri Masihi. Wanawali wote kumi pia walikuwa na mafuta taa.

5. Tukizungumza kwa lugha ya kiroho, taa inawakilisha nini? Zaburi 119:105.
6. Kwa kuwa neno ni taa, mafuta yanawakilisha nini? Ufunuo 3:18 (sehemu ya mwisho).
7. Ni nini utia wateule mafuta katika kipindi hiki? Matendo ya Mitume 10:38; 1 Yohana 2:27.

**Maelezo:** Kutokana na hili tunaona kwamba mafuta ni Roho. Wanawali hawa wote walikuwa wametiwa mafuta kwa Roho, lakini watano hawakuwa na upako wa kutosha. Tunasoma kwamba Mitume walikuwa wamepokea (au kutiwa mafuta) na wamejazwa na Roho na hivyo ndivyo mafuta ya ziada huifadhiwa. Wale ambao



**Maelezo:** Wanafunzi wake walikuwa wafuasi wake, na hivyo ndivyo ilivyo leo. Inafaa kuzifuata nyayo zake, na kufanya uthibitisho kamili wa utumishi wetu. Kwa uweza wa Roho tunaweza kuwa washindi wenyewe, na kushinda ulimwengu huu, kuishi maisha ya utauwa ambayo wengine watafuata. Tutapata furaha katika utoaji wa uwezo wetu na muda wetu katika kazi hiyo ambayo aliishi kufanya hadi kufariki.

7. Ni nia ipi inafaa kuwa ndani yetu? Wafilipi 2:4, 5.
8. Ni kanuni ipi ya msingi ambayo itafanya mfanyakazi wa kweli wa injili kupiga hatua? 2 Wakorintho 5:14, 15.
9. Kiasi chochote cha kazi, mateso au kujitolea yatatufaidi chochote bila upendo huu? 1 Wakorintho 13:1-3.
10. Tunatarajia kutendewa bora kutoka ulimwenguni kuliko jinsi Mwokozi wetu alivyopokelewa? Yohana 15:18-20.
11. Je, mateso kwa ajili ya Masihi ni sehemu ya kuishi duniani kwa waumini? Wafilipi 1:29.

*******************************

11. Yahshua alisema nini kwa mwanamke huyu kuhusu wokovu? Jinsi gani yeye alieleza kuhusu ibada ambayo hukubalika? Yohana 4:22-24.
12. Je, huyo mwanamke alisema nini kuhusu Masihi? Yahshua alifanya tangazo gani? Yohana 4:25, 26.
13. Wakati wanafunzi wa Masihi, ambao walikuwa wameendea chakula, waliporudi kwenye eneo la tukio na kumpa chakula, jibu lake lilikuwa lipi? Yohana 4:31-34.
14. Mwanamke huyo alifanya nini na nini ilikuwa matokeo ya ushuhudiaji binafsi wa Mwokozi? Huu ni mfano kwa ajili yetu? Yohana 4:25-30; 35-42.

*******************************

**Somo La Septemba 2, 2017.**

## KUITWA KWA KAZI MAALUM KWA WAKATI MAALUM

**Somo Kuu: Ufunuo sura ya 16.**
**Fungu La Kukariri: Ufunuo 16: 1.**

1. Ni juu ya nani ambaye pigo la kwanza kati ya yale mapigo saba ya mwisho lilimwagiwa? Ufunuo 14:9, 18: 4.
2. Ni ishara gani mbili zimepeanwa kwa wakati huu maalum wa maandalizi? Nahumu 2:3.
3. Kumekuwa na jumbe tatu kwa duniani yote ambazo zilitumwa tangu mwanzo wa injili. Ni nini na ni wakati upi ujumbe wa kwanza umetolewa? Ufunuo 14: 6.

**Maelezo:** Huu ulikuwa ujumbe uliotumwa mbele katika siku za Mitume, katika ulimwengu wa waabuduo sanamu ili kuharibu sanamu zao na kmwabudu yeye



11. Ni taarifa ipi maalumu Samweli alijulisha mfalme Sauli kuhusu kutii? 1 Samweli15:22.
12. Kwa nini Sauli alikataliwa na Elohim kama mfalme? Aya ya 23.
13. Je, neno la Bwana linatufundisha kwamba wasiotii wataadhibiwa hata katika maisha haya? Jinsi gani thawabu yetu itaamuliwa? Warumi 2:6-11.
14. Tumeshauriwa kufanya nini katika Waebrania 2:1-3?

*******************************

**Somo La Agosti 5, 2017.**

## MAHUBIRI JUU YA MLIMA

**Somo Kuu: Mathayo, sura ya 7**
**Fungu La Kukariri: Mathayo 7:21.**

1. Mwokozi alilaani mazoea gani mabaya? Mathayo 7:1-3.
2. Ni nini kwanza inafaa kufanyika kabla ya kujaribu kurekebisha wengine? Mathayo 7:4, 5; Mathayo 5:23, 24.

**Maelezo:** Ni ukosefu wa Roho ya kweli ya uvumilivu na upendo ambayo uongoza mtu kusisitiza makosa kwa wengine, na hufanya mlima kutoka kwa mlima wa fuko. Kulaumu na kuabisha kamwe hakujawahi kuokoa nafsi iliopotoka, lakini wengi hupotoka zaidi kwa hayo. Roho nzuri ya kukaripia kwa upole, kukaripia aliyekosea na kwa faragha kwa kuonyesha upendo wa huruma, ndiyo itaweza kumrejesha mtu katika njia nyembamba.

3. Ni nini imesisitizwa hapa kuhusu njia mbili za maisha, ambayo ni dhahiri leo? Mathayo 7:13, 14.



10. Ni ahadi gani nyingine inaonyesha kwamba anaongoza Israeli, uzao wake mteule? Isaya 59:20, 21; na Yeremia 31:35, 37.
11. Je, Bwana aliahidi kuwakusanya tena Israeli katika nchi ya ahadi kwa mara ya pili? Isaya 11:11-13.
12. Petro alisema nini? Kwa mujibu wa Mtume Petro, jinsi gani mataifa watabarikiwa kupitia familia hii teule? Matendo 3:22-25.
13. Wakati mataifa watakuja kupigana na Yerusalemu, nani ambao watakuwa wakiishi huko? Ezekieli 38:16.

*******************************

**Somo La 30 Septemba, 2017.**

## LENGO NA MADHUMUNI YA MAISHA

**Somo Kuu: Yohana 15:1-20**
**Fungu La Kukariri: Yohana 15:8**

1. Ni nini ilimfanya Baba kutoa mwana wake — na Yahshua alijitoa kwa hiari yake mwenyewe? 1 Yohana 4:10, 16; Yohana 10:10, 11, 15, 17.
2. Je, Masihi aliachana na starehe na utajiri ili afanye kazi yake? 2 Wakorintho 8:9; Luka 9:58.
3. Ulimwengu ulithamini kazi ya Masihi, hata kama alijitolea kwa yote? Yohana 1:11.
4. Kunaweza kuwa na upendo mkuu zaidi kuliko ule upendo ambao Masihi alionyesha kwa ajili yetu? Yohana 15:13; Warumi 5:7, 8.
5. Ni tuzo gani ambalo lilimtia moyo Bwana wetu kuvumilia mateso msalabani? Waebrania 12:12; Isaya 53:11, 12
6. Ni kwa nani Yahshua aliachia kazi yake? Marko 13:34.



hupokea Roho na kisha wasiendelee “kuenenda katika Roho” watakuwa kati ya wanawali wapumbavu, kwa sababu taa zao zitazimika.

8. Nini ilitendeka wakati Bwana arusi alipokawia? Mathayo 25: 5.
9. Ni nini ilisikika usiku wa manane? Mathayo 25: 6.
10. Waliamka kufanya nini? Mathayo 25: 7.
11. Wale wapumbavu waliazima nini? Mathayo 25: 8.
12. Walipata jibu lipi na ushauri upi? Mathayo 25: 9.

**Maelezo:** Haiwezekani kuazima imani na nguvu za kiroho kutoka kwa mtu mwingine. Lazima upate kutoka kwa Bwana. Mfano huu hasa unasisitiza umuhimu wa kuwa tayari katika nyakati zote na hatari ya kuzembea katika mienendo yetu ya kiroho. (Soma Mathayo 25: 10-13.)

*******************************

**Somo la Julai 8, 2017.**

## UJUMBE KWA MILIMA YA ISRAELI

**Somo Kuu: Ezekieli 36**
**Fungu La Kukariri: Ezekieli 36:24.**

1. Ni kwa nani ujumbe huu hasa ulitumwa? Ezekieli 36: 1.
2. Maadui walisema nini kuhusu milima ya Israeli? Ezekieli 36:2.
3. Huu ujumbe ni wa wakati wetu kufuatia kipindi cha ukiwa, au ni kwa muda katika siku zilizopita? Ezekieli 36: 3.
4. Huu ujumbe ni nini kwa milima ya Israeli? Ezekieli 36:4-7.

4. Kutakuwa na manabii wa uongo na walimu wa uongo katika siku za mwisho? Mathayo 7:15; Mathayo 24:24.
5. Ni jinsi gani tutawatambua? Isaya 8:20; Mathayo 7:16, 17.
6. Wahubiri wa uongo hukiri imani katika Mwokozi, na wanaweza kufanya kazi nzuri katika jina lake. Mathayo 7:22.
7. Hatima yao itakuwa ipi katika siku ya hukumu? Mathayo 7:23.
8. Je, Yahshua anasema nini kuhusu wale watakao ingia katika ufalme? Mathayo 7:21.
9. Anawalinganisha na nini wale husikia na kutenda aliyoyanena? Mathayo 7:26, 27.
10. Wale husikia tu wanalinganishwa na nini? Mathayo 7:26, 27.
11. Kumwamini mwana tu bila kutii kutatufanya tupate chochote? Yakobo 2:19, 20; Yakobo 1:21, 22.

******************************

**Somo La Agosti 12, 2017.**

## HAKIMU WA DUNIA YOTE

**Somo Kuu: Mwanzo 18:16-33.**
**Fungu La Kukariri: Mwanzo 18:25.**

1. Katika uharibifu wa Sodoma na Gomora, ni nini imesemwa kuhusu wenye haki kuepuka hukumu? Mwanzo 18:23-32.
2. Nini imesemwa kuhusu miji hiyo kuwa mifano ya hukumu ya baadaye? 2 Petro 2:6.



6. Ni wapi ambapo Bwana alisimama wakati alipokuwa akipitia Samaria? Yohana 4:4-7.

**Maelezo:** Wakati Mwokozi alipokuwa akielekea Galilaya, maili 100 kaskazini ya Yerusalemu, alisimama katika Samaria katika bonde nzuri linaloelekea mashariki kwenye mto Yordani. Hapa alipata kisima cha Yakobo, ambapo alikuwa amechoka akaketi chini kupumzika. Kulikuwa na uwezekano kwamba alikuwa mdhaifu wa uchovu na kuwa na kiu baada ya safari ndefu.

7. Jinsi gani Mwokozi alianzisha mazungumzo na mwanamke kisimani? Mstari wa 7.
8. Jinsi gani mwanamke alimpokelea, na ni nini kile kilichoonekana kuwa kwa wingi kwenye moyo wake? Yohana 4:8, 9.
9. Jinsi gani Yahshua aliyageuza mazungumzo ili kumpa mahitaji yake ya kiroho? Yohana 4:10-14.

**Maelezo:** Huu ni mfano bora kwetu sisi kuufuata. Kwa nyakati zote tunapaswa kuyageuza mazungumzo yetu ili kuwasaidia kiroho na kuwapa mahitaji ya milele ya wale ambao sisi hukutana nao.

10. Jinsi gani Yahshua alithibitisha kwa mwanamke huyu kwamba alikuwa tofauti na mtu wa kawaida? Yohana 4:16-18.

**Maelezo:** Ingawa sisi hatuna uwezo wa kuwaambia watu kuhusu maisha yao wenyewe kama Masihi alivyokuwa, tunaweza kuwaambia kuhusu hali ya ulimwengu; Hali ambayo kwa kimiujiza hutimiza maneno ya manabii wa kale.



5. Ahadi kwa milima ya Israeli kwa wakati huu, na siku za usoni ni zipi? Watu watamiliki nini kutoka kwa hiyo milima? Ezekieli 36: 8-10.
6. Nini imesemwa kuhusu jinsi Israeli wanavyofanyiwa wakati huu? Watatendewa sawa kama mbeleni au bora? Ezekieli 36:11.
7. Nchi hii itawahi kuwa ukiwa tena? Ezekieli 36:12.
8. Nini ilisema kuhusu Israeli kuitia nchi uchafu, na kuhusu adhabu yao kwa ajili ya dhambi zao? Ezekieli 36: 17-20.
9. Je, Baba alikuwa na huruma juu ya Israeli, na ni baraka wakati huu katika kuwakusanya Wayahudi tena Israeli, ni kwa sababu ya haki yao wenyewe? Ezekieli 36:22, 32
10. Kutakuwa na mabaki ya watu hawa yaliyotengwa kwa ajili ya matumizi takatifu (kutakaswa), na ni jinsi gani kazi hii ilikuwa iaanze nao? Ezekieli 36: 23, 24; Warumi 9:27, 28.
11. Baba anasema nini kuhusu umiliki wa ardhi ambapo sasa wanakusanywa? Je, hii ardhi ni ya Israeli? Ezekieli 36:24.
12. Nyoyo zao zitabadilishwa kutoka kwa nyoyo za jiwe wawekwe nyoyo za nyama kabla kukusanywa au ni baadaye? Ezekieli 36:24-27.
13. Ni vipi kuhusu baraka juu ya nchi katika kuifanya iwe na mazao, na hii itakuwa na athari juu ya watu katika kukumbuka dhambi zao, na matendo yao maovu? Ezekieli 36:30, 31
14. Katika siku ile wao watakuwa wanatakaswa maovu yao, kupitia kupokea Roho, watakuwa wakijenga mahali palipoharibiwa na miji ya kale, na nchi itafanana na bustani la Edeni? Ezekieli 36:33-36.



**Somo La Septemba 23, 2017.**

## MBEGU YA KIFALME AMBAYO BWANA AMEBARIKI

**Somo Kuu: Isaya 61**
**Fungu La Kukariri: Isaya 61: 9.**

1. Ni ahadi ipi alipewa mama Hawa? Mwanzo 3:15.
2. Ni ahadi gani ipi ilifanywa kwa uzao wa Ibrahimu, na ni kwa nini? Mwanzo 22:17, 18; Mwanzo 26: 4, 5.
3. Ni kwa umbali gani Baraka za Ibrahimu zilikuwa zifikie, na wengine pia walikuwa wabarikiwe kupitia uzao wake? Mwanzo 12:2.
4. Je, Muumba anasema nini zaidi kuhusu familia hii? Isaya 61:3.
5. Baba alitarajia baraka kuchipuka na kukua? Isaya 61:11.
6. Israeli kwa wakati wote walikuwa waminifu kwa tumaini lililotolewa kwao? Yeremia 2:21, 22.
7. Je, Yeye bado alitoa wito kwa uzao wake mteule kurudi kwake kwa njia ya kiroho na kutubu? Yeremia 4:1-4.
8. Je, walitubu na matokeo yalikuwa yapi? Yeremia 5:11-15; Ezekieli 22:19-22.

**Maelezo:** Unabii huu ulitimia kwa njia ya kusikitisha baada urejesho wa kwanza wa Israeli, na ujenzi wa hekalu la pili. Ni uharibifu huu Mwokozi wetu pia alitangaza. Tito jenerali wa Kirumi katika mwaka wa 70 A.D aliuzingira na kuuteka mji wa Yerusalemu.

9. Je, yeye bado ana kusudi la kuhifadhi uzao wa Israeli? Isaya 49: 8: 48:10-12.

**Maelezo**: Kama mtu atatafuta haki kwa dhati, basi ni lazima kujivika haki ya Masihi, hivyo mtu hufungua mlango na kumkaribisha Masihi. Soma Ufunuo 3:20.

8. Kama mtu atajaribu kutegemea haki yake pekee, atafanya nini? Warumi 10:1-3; Isaya 64: 6.

9. Je, tutahofu kwamba mzigo utakuwa mkubwa sana? Mathayo 11:29, 30; 1 Petro 5:7.

10. Baada ya kupata njia ya kweli ya haki, maisha yetu yatakuwa na faida kwa Baba katika kuvuta nafsi za watu? Yohana 15:1, 2.

*******************************

**Somo La Agosti 26, 2017.**

## MWOKOZI, MFANYAKAZI WA KIBINAFSI

**Somo Kuu: Yohana 4:1-42**

**Fungu La Kukariri: Yohana 4:22, 23.**

1. Nani ambaye alikuja kwake Yahshua usiku? Yohana 3:1, 2.

2. Jinsi gani Yeye alitaja hitaji la nafsi kwa huyo mtawala, na ni haja gani muhimu ambayo yeye alisisitiza? Yohana 3:3-5.

3. Mwenye dhambi anaweza kujipa wokovu wake mwenyewe au yeye anahitaji msaada? Yeremia 13:23; Warumi 8:6-7.

4. Ni kutoka wapi nguvu za kiroho na msaada hupatikana? Luka 11:9, 10.

5 Ni mfano gani hutumika kuonyesha utayari wa Baba kutupea msaada wakati wa tunapohitaji? Luka 11:11-13.



3. Tunafaa kuhofu au tunafaa kuuliza swali juu ya hukumu ya Baba yetu wa Mbinguni? Zaburi 96:10; 1 Yohana 4:16-18.

4. Tunafaa kuogopa vile watu wanaweza kutufanyia, au badala yake kuchagua kuanguka katika mikono ya Baba wa mbinguni mwenye huruma? 2 Samweli 24:13, 14.

**Maelezo:** Daudi kutoka akiwa kijana, hakuishi kwa ajili yake mwenyewe. Madhumuni ya maisha yake bila hofu ya vile adui angeweza kufanya, ilikuwa ni kuwabariki wengine. Yeye alikuwa na ushahidi wa uwepo wake na mkono wenye nguvu za kuleta ukombozi. Akamwua simba na dubu, (1 Samweli 17:34-36), na akawa na nguvu juu ya jitu kubwa la Wafilisti, (mistari 48, 49), — hakuogopa kile watu wangefanya.

5. Wakati uwepo wa Baba hu pamoja nasi, mambo yataenda vizuri kila wakati? Waebrania12:6, 1 Petro 1:7.

6. Vipi kuhusu Ayubu aliyepoteza mali yake, na watoto wake wote? Ayubu 1:20-22.

7. Wakati mwili wake uliteseka sana, alipoteza imani na kulalamika? Ayubu 7:20, 21.

**Maelezo:** Ni vizuri kutambua maisha ya unyenyekevu wa Mwokozi, na tazama umaskini wake; Mateso yake katika Gethsemani; Kuaibishwa mbele ya waliomdhihaki; taji la miiba mikali juu ya kichwa chake; Kesi na hukumu mbele ya watu waovu kama mhalifu na uchungu wake juu ya msalaba. Lakini kwa hayo yote aliibuka kuwa mshindi, na kuinuliwa mbele ya mkuu sana wa mbinguni, na kupewa taji kama mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana.



katika maisha yake kwa ajili ya utukufu wa Elohim? Mathayo 25: 24-28.

8. Badala ya kuingia katika ufalme, ni nini itasemwa kwa mtumishi asiye na faida ambaye huficha maisha yake yote katika dunia hii ya kale? Mathayo 25: 29-30.

**Maelezo**: Hivi ndivyo mamilioni wanafanya leo, kuishi kwa ajili yao wenyewe, na kuzikwa ndani kabisa katika mambo ya dunia. Wanatafuta pesa, mali, na raha, kuabudu dola tu na kile ambacho dola hutoa kwao. Mwisraeli wa kweli si hivyo. Yeye anafaa kukuza talanta yake na kuishi maisha yake kwa ajili ya ongezeko la ufalme, kutoa zaka na sadaka, na pia kuishi katika utiifu wa upendo, na kujitenga mwenyewe na ulimwengu.

9. Katika kufuata hatua za Mwokozi wetu, ni mambo ya nani yatakayotuhusu sisi zaidi? Luka 2:49.

10. Kuna kitu cha thamani zaidi kuliko chakula kwa ajili ya mwili na mavazi, ni nini lazima itabaki kwanza kabisa katika kila nyoyo? Luka 12:23-32.

11. Ni nini kitatokea daima kwa maisha ya kiroho ya mtu asiye na faida ambaye huficha talanta yake, na kushindwa kutoa mazao? Luka 13:6-9.

12. Ni nini daima itatokea kwa mtu ambaye huweka katika akiba kwa ajili yake mwenyewe, na kuzika talanta yake katika ardhi, na si tajiri kwake Elohim? Luka 12:16-21.

*******************************



15. Ni tukio gani Mtume Paulo alishirikisha na kupokelewa kwa Israeli tena? Warumi 11:15-21.

*******************************

**Somo La Julai 15, 2017.**

## SHERIA YA ROHO WA UZIMA

**Somo Kuu: Luka 6:17-40.**

**Fungu La Kukariri: Luka 6:19.**

1. Ni kutoka miji gani watu walikusanyika pamoja? Luka 6:17.

**Maelezo**: Walikuwa wametoka umbali wa maili 50 au zaidi, hii ilikuwa juhudi kubwa sasa kwa sababu siku zile kutembea ilikuwa njia kuu ya usafiri.

2. Nini imesemwa kuhusu wagonjwa wote katika ule umati mkubwa wa watu? Luka 6:18, 19.

3. Jinsi gani Mwokozi alijiandaa kwa ajili ya mkusanyiko huu mkubwa? Luka 6:12.

4. Baada ya kushinda usiku katika maombi, mwili wake ulipata nguvu kutokana na nini? Luka 6:19.

5. Mtume Paulo pia alikuwa amejawa na wema huu wa nguvu za uponyaji? Matendo 19:11, 12.

6. Tukijua kwamba miujiza hii ya ajabu iliandilwa kwa ajili yetu, nini tumeamrishwa kufanya? 1 Wakorintho 11:1.

7 Ili kufanya mambo haya yote leo, nini itakuwa muhimu? 1 Wakorintho 1:5; 2 Wakorintho 8:7.

8. Tukitajirika katika yeye, katika maarifa na maneno, matokeo yatakuwa yapi? 2 Wakorintho 8:7-14.

**Maelezo:** Ni Shetani hupoteza watu katika mazungumzo yao, na husababisha wao kupata aibu kwa

8. Ayubu alielewa sababu ya mateso haya, au alijaribu kujifanya kuwa mwenye haki? Ayubu 31: 3-7, 24-27, na 29, 30.
9. Nani ambaye alikuja kwa Ayubu na maneno ya faraja, na kutamka unabii ambao ulitimizwa baadaye? Ayubu 32: 5-10
10. Baadhi ya maneno hayo ya faraja yalikuwa yapi? Ayubu 33: 22-29.
11. Katika kujisalimisha na unyenyekevu wake, Ayubu hatimaye alisema nini? Ayubu 40: 3, 4; 42: 1-6. Tafadhali Soma 1 Petro 4:12, 13, na 5:6, 7.
12. Ni nini imesemwa kuhusu mtu yule ambaye huadhibiwa na Baba? Zaburi 94:2-15.
13. Ni amri gani ilitolewa kwa wale watu watatu, —Ayubu angefarijiwa? Ayubu 42: 7-9.

**Maelezo:** Watu hao watatu ambao walikuja kama marafiki wa Ayubu walimhukumu visivyo katika kipindi cha dhiki yake. Ghadhabu ya Elohim ikawaka juu yao. Gadhabu haikuondolewa hadi Ayubu alipoomba kwa ajili yao.
14. Baada Ayubu kuvumilia kwa subira, na kuomba kwa ajili ya marafiki zake, alibarikiwa vipi? Aya ya 10-16.
15. Ni nini imesemwa kuhusu rehema na hukumu katika Yakobo 2:12, 13?
16. Mtoto Samweli alipoachishwa maziwa, na mama yake kumpeleka mbele ya Eli kuhani. Ni maneno gani ya kinabii aliyoyazungumza kuhusu hakimu wa dunia? 1 Samweli2:10.
17. Je, mfalme Daudi aliutaraji sana wakati huo? Zaburi 94:1-3; 96:10-13.



18. Je, hitimisho ya yote ambayo yanatarajiwa kutoka kwa wanadamu ni ipi, na je, hakimu Mkuu anajua yote yaliyo sirini? Mhubiri. 12:13, 14.

*******************************

**Somo La Agosti 19, 2017.**

## UKOMBOZI KUPITIA KUJITOLEA KWA ROHO

**Somo Kuu: Warumi 6**
**Fungu La Kukariri: Warumi 6:16.**
1. Kwa nini mabadiliko ni muhimu katika asili ya mwanadamu? Warumi 7:8, 9.

**Maelezo:** Kuwa na umwili ina maana kuwa na hali ya kimwili au katika hali ya asili ya mtu.
2. Ni ushauri gani bora Hezekia aliwapa watu katika nyakati zake? 2 Mambo ya nyakati 30: 8.
3. Ni nini ubadilika ndani ya nafasi zetu wakati huwa tunajitolea kwa Baba? Warumi 6:13, 14.
4. Je, hii inamaanisha kuendelea katika dhambi? Warumi 6:15.
5. Kwa nini ni muhimu sana kwamba tujitolee kwa Muumba badala ya kujitolea kwa nguvu za uovu? Warumi 6:16; Mathayo 6:24.
6. Matokeo yatakuwa yapi tukijitoa kwake? Warumi 6:11; 1 Petro 2:24; Waebrania 9:14, 15.
7. Mwokozi alitoa ahadi gani nzuri kwa wale ambao wataenda kwake? Mathayo 11:28 na sehemu ya mwisho ya 29.



sababu ya mtu fulani. Wakati unaweza kusema chochote ambacho si kweli kuhusu mtu, una hatia ya kuaibika (Zaburi 15:1-3.) Wakati tunatajirishwa na Bwana, tukitafuta Roho Mtakatifu, na kujitenga na waongeao maovu, basi tutakuwa washiriki wa tabia ya kiroho na kujazwa na wema wa mbinguni.
9. Je, mtazamo wetu unapaswa kuwa upi dhidi ya maadui zetu na kwa wale hutuchukia na kutulaani? Luka 6:27, 28.
10. Ikiwa mtu atakupiga ama kukutishia au kusema uongo kukuhusu wewe, utawafanyia kama walivyokufanyia? Luka 6:29-31.
11. Ni kwa njia gani mtumishi wa kweli atakuwa tofauti na watu wale wasiomcha Elohim ambao ni wa dunia? Luka 6:32-34.
12. Ni ahadi gani imetolewa kwa wale ambao wana mawazo sahihi na nia nzuri kwa maadui zao? Luka 6:35.
13. Ni vipi kuhusu kutoa kwa wanaohitaji, na kutoa kwa ajili ya kuendeleza injili? Luka 6:36-38.

*******************************

**Somo La Julai 22, 2017.**

## MAWAIDHA KWA WAUMINI

**Somo Kuu: Yohana 12**
**Fungu La Kukariri: Yohana 12:35.**
1. Je, wanafunzi walielewa zaidi mambo aliyowaambia Mwokozi? Yohana 12:24-31.
2. Ni nini lazima sisi tuwe waangalifu katika siku hizi za mwisho? 1 Petro 5:8.



14. Katika wakati mkubwa wa taabu ni nani atakuwa mlinzi wetu? Zaburi 91:9, 10, 11

*******************************

**Somo La 16 Septemba, 2017.**

## WITO WA WATUMISHI NA USAMBAZAJI WA KARAMA

**Somo Kuu: Mathayo 25: 14-46.**
**Fungu La Kukariri: Mathayo 25: 19.**
1. Ni kwa nini ufalme wa Mbinguni unalinganishwa na ni nani ambaye alitembea kwenda nchi ya mbali? Mathayo 25: 14.

**Maelezo:** Masihi bado anaita watumishi kufanya kazi yake.
2. Ni nini imesemwa kuhusu usambazaji wa talanta, au karama kwa ajili ya kuongeza kundi, na kuzivuta nafsi za watu? Mathayo 25: 15.
3. Ni nini mtumishi alifanya yule ambaye alipokea idadi kubwa ya talanta? Mathayo 25: 16, 17.
4. Ni nini mtumishi alifanya yule ambaye aliyeipokea talanta moja? Mathayo 25: 18.
5. Nini kinachotokea baada ya muda mrefu? Mathayo 25: 19.
6. Je, ni tuzo lipi kwa wale ambao hutumia sahihi talanta walizopokea, na kuziongeza kwa ajili ya kuzivuta nafsi? Mathayo 25:20-23.
7. Je, ni zawadi gani aliyopewa mtumishi ambaye alificha talanta yake katika ardhi, kutokuwa na ongezeko lolote